TAFSIRI RAHISI YA MALENGO YA

MKUKUTA II

MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI - II

Juni 2011

policy forum

YALIYOMO **Uk.**

1.0 UTANGULIZI iii

2.0 USULI iv

3.0 SHUKRANI iv

4.0 LENGO LA KITABU HIKI v

SEHEMU YA I

5.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MKUKUTA I 1

6.0 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA MKUKUTA I 3

SEHEMU YA II

7.0 MISINGI NA NGUZO ZA MKUKUTA II 5

8.0 VIPAUMBELE NA MALENGO YA MKUKUTA II 7

9.0 MPANGO WA UTEKELEZAJI 9

10.0 USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MKUKUTA II 12

11.0 USIMAMIZI WA FEDHA 12

12.0 MAJUKUMU NA WAJIBU WA MWANANCHI 13

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini – II

Kitabu hiki kimetayarishwa na *Lilian R. Kallaghe* kwa niaba ya Policy Forum na kuhaririwa na Sekretarieti ya Policy Forum.

Picha zote na: Mpoki Bukuku

Toleo la kwanza 2011

ISBN: 978–9987–708–01–7

Kimesanifiwa na kupigwa chapa na;
Tanzania Printers Limited
P.O. Box 451 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 286 6776–80

1.0 UTANGULIZI

Je, ni kwa kiwango gani unashiriki katika kuandaa, kuelewa na kufuatilia utekelezaji wa sera mbalimbali zinazohusu maisha na jamii yako kwa ujumla? Na je, ushiriki wa mwananchi wa kawaida katika masuala ya sera una umuhimu gani?

Wananchi wengi wamekuwa na dhana kwamba uundaji na utekelezaji wa sera ni kazi ya wanasiasa na serikali. Ni katika kuamini hivyo, baadhi ya wananchi wamejikuta wakipoteza fursa na haki yao ya kushiriki katika kujiletea maendeleo, huku wakiwaachia watendaji jukumu la kufanya maamuzi muhimu yanayogusa maisha ya jamii.

Kwa upande wa pili, sera nyingi zimekuwa zikiandaliwa kwa njia ambayo si shirikishi. Na hata pale ambapo wananchi wameshiriki katika kuandaa ama kutoa maoni yao, sera hizo hurudishwa kwa jamii zikiwa zimejazwa takwimu, maneno mengi na kuandikwa kwa lugha ngumu ambayo si rahisi kwa mwananchi wa kawaida kuielewa.

Kitabu hiki kimeandaliwa na Policy Forum kutoka kwenye ripoti rasmi ya MKUKUTA awamu ya II, iliyochapishwa na serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi (Julai 2010).

Ni matarajio yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa chachu ya kuongeza ufahamu, uelewa na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa MKUKUTA II. Tumia kitabu hiki kuuliza maswali, kuanzisha mijadala ya kijamii katika ngazi ya kitongoji, vijiji, kata, tarafa, wilaya hadi taifa.

Policy Forum inaamini kwamba ushiriki wa wananchi wenye uelewa mpana na wa kina kuhusu sera mbalimbali ni muhimu katika kuandaa mipango ya maendeleo yao, kuhakiki matumizi ya bajeti iliyotengwa, utekelezaji wa vipaumbele walivyopanga, kufuatilia na kudai uwajibikaji wa viongozi wao na hatimaye kukuza uchumi wa kipato na kujiletea maendeleo.

Kitabu hiki kinaelezea kwa ufupi tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, maarufu kama MKUKUTA, misingi au makundi ya vipaumbele, mafanikio na changamoto za MKUKUTA I, kwa kipindi cha kati ya miaka 2005/06-2009/10.

Vilevile kinaelezea misingi/makundi na malengo muhimu yaliyopewa kipaumbele na yatakayoendelezwa katika utekelezaji wa awamu ya pili ya MKUKUTA- (MKUKUTA II), ulioanza kutekelezwa rasmi mwaka 2010/11 na 2014/15.

2.0 USULI

MKUKUTA ni nini? Ni kifupisho cha maneno ya Kiswahili yenye maana ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania.

MKUKUTA awamu ya I (2005/06-2009/10) ulilenga katika kukuza uchumi, kupunguza umaskini wa kipato, ubora wa maisha ya watu na ustawi wa jamii pamoja na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji. Utekelezaji wake ulienda sambamba na uandaaji wa ripoti za kila mwaka zikiainisha uzoefu, mafunzo, mafanikio na changamoto.

Kila mwaka, ripoti hizo zilijadiliwa na wadau mbalimbali katika makongamano na mikutano ya kitaifa ya sera. Maoni kutoka kwenye mapitio na mijadala hiyo yalitumika katika kuboresha mpango wa mwaka uliofuata.

MKUKUTA inachangia katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2015).

3.0 SHUKRANI

Kitabu hiki kimetayarishwa na *Lilian R. Kallaghe* kwa niaba ya Policy Forum. Tunatoa shukrani za pekee kwa Umoja wa Nchi za Ulaya ambao wamefadhili uchapishaji wa kitabu hiki na wafadhili wengine wa mfuko wa Policy Forum.

Wengine waliochangia maoni yao katika kuboresha kitabu hiki ni Sekretarieti ya Policy Forum ambao pia waliandaa taarifa mbalimbali na kutoa maoni yao wakati wa kuandaa kitabu hii.

Picha zimepigwa na Mpoki Bukuku. Policy Forum inaishukuru Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuchapisha na kusambaza ripoti ya MKUKUTA II ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa katika uandishi wa kitabu hiki.

4.0 NINI LENGO LA KITABU HIKI?

Lengo la chapisho hili ni kuongeza uelewa na ujuzi wako kuhusu MKUKUTA, kukuhamasisha na kukupa sauti zaidi ili uweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Ushiriki wako utakuwezesha kuongeza kipato chako kuanzia ngazi ya familia, jamii na hatimaye kukuza uchumi wa taifa na kuleta maendeleo kwa ujumla.

Ili kusaidia kukuza uelewa wako, muhtasari huu usio rasmi umeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo ni rahisi kuelewa. Ni matarajio ya Policy Forum kwamba utatumia kitabu hiki kama chachu ya kufuatilia na kuhoji utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kudai uwajibikaji wa viongozi wa ngazi zote.

Tunatarajia pia kuona na kusikia mijadala endelevu ya kijamii ikianzishwa kuanzia ngazi ya kitongoji, vijiji, kata, tarafa, wilaya hadi taifa. Ushiriki wako utachangia katika kuleta maendeleo na kupunguza umaskini wa Tanzania!

SEHEMU YA I

5.0 TATHMINI FUPI YA UTEKELEZAJI WA MKUKUTA I

Tathmini ya uchumi ikilinganishwa na kukua na kupungua kwa umasikini nchini ilifanyika baada ya utekelezaji wa MKUKUTA I. Tathmini hiyo ilifanyika kwa kuzingatia **makundi makuu matatu** ya malengo ya maendeleo;

5.1 Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

5.2 Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii.

5.3 Utawala bora na Uwajibikaji.

5.1.1 Umaskini wa kipato na changamoto za mgawanyo wa mapato

Kwa ujumla, umaskini wa kipato uliendelea kupungua kwa kiwango kidogo sana. Kwa mfano, kwa kila watanzania mia moja, 36 kati yao walikuwa maskini katika miaka ya 2000/01 ikilinganishwa na 34 kwa mwaka 2007. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi unaotajwa hauwagusi wananchi wengi.

Katika kundi hili, maeneo yaliyopewa kipaumbele yalikuwa ni *Kilimo, Uvuvi, Viwanda na Uzalishaji.*

Wanawake ni mojawapo ya makundi yanayopata kipato cha chini

Mengine ni Madini, Ardhi, Utalii, Miundombinu na Mfumuko wa bei ambao umeripotiwa kupanda hadi asilimia 12.1 kufikia Desemba 2009, kutokana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani.

5.2 Kundi II: Kuboresha hali ya Maisha na Ustawi wa Jamii

Katika kundi hili, ilidhihirika kuwa mgawanyo wa fursa na rasilimali za nchi usio sawa uliendelea kusababisha umasikini. Mfano, kuna tofauti kubwa ya viwango vya umaskini miongoni mwa mikoa na baadhi ya wilaya zilizoko pembezoni mwa nchi. Tofauti za kijiografia na miundombinu mibovu vimechangia ukuaji mdogo wa uchumi na pato la mwananchi kwenye baadhi ya wilaya na mikoa. Katika kundi hili, utekelezaji ulilenga kufikia malengo yafuatayo;

1. Kuongeza ubora wa maisha na ustawi wa jamii, hususan kwa watu masikini zaidi, wanawake, wanaume, wazee, vijana, wenye ulemavu na makundi tete yaliyoachwa pembezoni.

2. Kuleta usawa katika upatikanaji wa elimu, haki ya kuishi na afya kwa wote bila kujali kipato, umri, jinsia na mengineyo.

Taarifa zilizotolewa zimeonesha mafanikio na changamoto katika utoaji wa huduma hasa kwa upande wa elimu, afya, maji, usafi wa mazingira, makazi bora na ulinzi wa jamii. Kuwekeza rasilimali zaidi katika elimu na afya kumeiwezesha nchi kutoka kwenye kundi la nchi za mwisho na kuingia kundi la kati. Tanzania imeshika nafasi ya 151 (2009) kutoka nafasi ya 163 (2000), kwa mujibu wa *Ripoti ya Upimaji wa Maendeleo ya Binadamu***.**

Kwa upande wa Kinga ya Jamii na Makundi Maalum, serikali imeandaa mfumo unaotambua makundi tete katika jamii. Makundi hayo ni watu wenye ulemavu, watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu na watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Wengine ni wazee wenye umri zaidi ya miaka 60, vijana, wajane na wasichana waliojifungua katika umri mdogo.

5.3 Kundi III: Utawala Bora na Uwajibikaji

Katika MKUKUTA, utawala bora unamaanisha mfumo wa sheria ambao ngazi zote za uongozi serikalini zinapaswa kuufuata kwa uadilifu. Lengo ni kulinda haki, usawa, kusimamia rasilimali za nchi na kuepuka matumizi mabaya ya mamlaka. Mkakati wa

utekelezaji wa nguzo hii ya MKUKUTA ulilenga kuona matokeo makuu yafuatayo:

- Utawala bora na utawala wa sheria unakuwepo.
- Viongozi na watumishi wa umma wanawajibika kwa wananchi.
- Uvumilivu wa kisiasa, kijamii na demokrasia unaendelezwa.
- Amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano vinahimizwa na kuendelezwa.

6.0 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA MKUKUTA I

Mafanikio:

Utekelezaji wa MKUKUTA I ulikuwa na mafanikio na changamoto zake. Baadhi ya mafanikio yaliyoripotiwa ni;

- kukua kwa uchumi kwa asilimia 7 tangu mwaka 2005 ikilinganisha na matarajio ya kati ya asilimia 6 hadi 8 kwa mwaka,
- kuboreshwa kwa huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji, nishati, mawasiliano na miundombinu, hususan barabara,
- mapato ya serikali kwa mwezi yaliongezeka kutoka wastani wa shilingi za Tanzania bilioni 177 mwaka 2005/06 hadi kufikia shilingi bilioni 390 mwaka 2009/10 na
- utawala bora na uwajibikaji- kumekuwa na ufuatiliaji wa karibu wa matumizi ya fedha za umma hasa kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Changamoto:

Ukuaji wa uchumi uliathiriwa na vikwazo mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi;

- mtikisiko wa uchumi wa dunia ulisababisha kupungua kwa mitaji na vitega uchumi na pia kupungua kwa idadi ya watalii wanaotembelea nchini.
- kupanda kwa bei ya mafuta duniani kumeongeza ugumu wa maisha na kusababisha mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali na hasa vyakula.
- ukame ambao haujawahi kutokea katika miongo (kipindi cha miaka kumi) ya karibuni. Hali hiyo ilitikisha uchumi kwani iliathiri zaidi sekta ya kilimo, mifugo na uzalishaji wa umeme nchini.

Changamoto za kitaifa zilikuwa;

- ushiriki na ushirikishwaji mdogo wa wananchi na wadau katika kupanga mipango ya uchumi na maendeleo,
- uimarishaji wa mifumo ya usimamizi wa rasilimali za umma,
- udhaifu katika kupanga vipaumbele na uratibu wa utekelezaji,
- kuwepo kwa idadi ndogo ya rasilimali watu na fedha katika sekta zote,
- kiwango cha chini cha ubora wa huduma zinazotolewa kwa jamii; maji, elimu, afya,
- sekta ya kilimo; udhaifu katika kusimamia uzalishaji, kusindika mazao ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini.
- kutokuwa na mipango na mikakati thabiti,
- ujuzi na utaalamu mdogo katika kuandaa, kusimamia na kupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA I.

Huduma ya maji safi mijini na vijijini ni mojawapo ya changamoto za kitaifa.

SEHEMU YA II

7.0 MISINGI NA NGUZO ZA MKUKUTA II

Mwaka 2000/10, serikali iliwashirikisha wadau mbalimbali katika kufanya utafiti, mijadala na mapitio ya MKUKUTA I kama sehemu ya maandalizi ya MKUKUTA II. Mijadala hiyo, pamoja na mambo mengine, iliainisha vipaumbele na namna ya kuimarisha na kuboresha mkakati wa utekelezaji wa MKUKUTA II.

Kwa kuanzia, **misingi** inayosimamia utekelezaji wa MKUKUTA II imetajwa kuwa ni;

1. Umiliki wa kitaifa; kwa maana ya wananchi wenyewe, serikali, mashirika ya hiyari, sekta binafsi na wadau wengine.
2. Kuwepo utashi wa kisiasa, viongozi bora na kuimarisha

uwajibikaji.

3. Kuunganisha uchumi wa wazalishaji wakubwa na wadogo.
4. Kuimarisha na kusisitiza ukuaji wa uchumi unaomlenga mtu maskini.
5. Kuunganisha mikakati ya kisekta inayoendana.
6. Kuendeleza rasilimali watu kwa usawa.
7. Kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa.
8. Kuimarisha ushiriki wa wananchi na jamii.

Tofauti na mpango wa awali, MKUKUTA II itasimamia zaidi kwenye jukumu na ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na kuongeza ajira. Hivyo basi **nguzo** kuu zitakuwa ni;

1. *Ufanisi katika matumizi na kuendeleza vitendeakazi vya uzalishaji ikiwemo mitaji na rasilimali watu:* Rasilimali nyingine muhimu katika uzalishaji ni pamoja na maji, ardhi, madini, misitu wanyama pori na uvuvi. Mkakati wa kuongeza uzalishaji utalenga kwenye kuendeleza ardhi, utafutaji na uchimbaji madini na matumizi ya teknolojia mpya. Kwa upande wa rasilimali watu, mkakati ni kuboresha utoaji mafunzo, elimu na ujuzi na pia kuendeleza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).

2. *Kuongeza ufanisi katika taasisi za umma:* Taasisi zinazofanya kazi kwa ufanisi ni muhimu katika kukuza masoko, utoaji wa huduma bora na masuala ya utawala. Ili kupata matokeo mazuri, mkakati wa hili unalenga kwenye kuimarisha utekeleza wa mfumo wa maboresho ulioanzishwa na serikali katika MKUKUTA I.

3. *Maendeleo ya Miundombinu:* Mkakati unasisitiza kwamba maendeleo ya miundombinu ndiyo kiini cha mchakato wa ukuaji uchumi. Miundombinu imara inapunguza gharama za kufanya biashara, kuvutia uwekezaji, kukuza uzalishaji, faida na kuongeza ajira. Vile vile inaboresha huduma za jamii, kuunganisha masoko na kusaidia kuleta usawa katika mgawanyo wa rasilimali. Hivyo basi, maendeleo ya nishati, barabara, reli, mawasiliano, bandari, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vitaendelea kupewa kipaumbele.

Miundombinu ndiyo kiini cha mchakato wa ukuaji uchumi.

4. *Usimamizi makini wa uchumi:* Mkakati huu umeelekezwa zaidi katika sera na taasisi zinazotoa maamuzi yahusuyo usimamizi bora wa fedha za umma. Hivyo basi, mkazo utakuwa kwenye kuainisha majukumu ya sekta binafsi na serikali, kuunda sera kwa njia shirikishi na kutoa maamuzi kwa uwazi zaidi.

5. *Utafutaji rasilimali fedha:* Kwa ujumla, upatikanaji fedha unatarajiwa utokane na mapato ya serikali (kodi), mikopo na ruzuku. Michango mingine inayotarajiwa ni ile ya jamii, sekta binafsi (wawekezaji wa ndani na nje) na wadau wa maendeleo.

8.0 VIPAUMBELE NA MALENGO YA MKUKUTA II

Makundi yote makuu matatu ya MKUKUTA yameendelea kupewa kipaumbele katika utekelezaji wa awamu ya pili: *(i) Kukuza Uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, (ii) Kuongeza ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii na (iii) Utawala bora na Uwajibikaji.*

8.1 Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato

Katika awamu hii, kundi hili litalenga kwenye mambo yafuatayo:

- Kuongeza ajira endelevu.
- Kuboresha miundombinu hasa barabara za vijijini, reli, nishati na maji ili kukuza uzalishaji.
- Kuhimiza ushiriki wa wadau katika uzalishaji.
- Mgawanyo sawa wa mapato yatokanayo na rasilimali za umma.
- Kuongeza kipato kwa makundi mbalimbali ya kijamii; wanawake, vijana na makundi mengine yaliyoachwa pembezoni.
- Kutoa fursa za kuchangia ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira na pato la watu masikini katika sekta za kilimo, utalii, madini na uzalishaji.

8.2 Kuongeza Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii

Mkazo katika kundi hili utakuwa ni kuhakikisha kwamba huduma bora za jamii zinawafikia walengwa; watu masikini na makundi ya watu wasiojiweza. Huduma hizo ni muhimu pia ziendane na ongezeko la idadi ya watu.

Malengo katika kundi hili yamewekwa katika:

- Kuboresha elimu.
- Afya na lishe bora.
- Upatikanaji wa maji safi na salama, usafi na uhifadhi wa mazingira.
- Ulinzi wa haki za makundi maalum na watu wasiojiweza katika jamii.
- Utoaji wa huduma bora za jamii kwa wote .

8.3 Utawala bora na Uwajibikaji

Utawala bora na uwajibikaji ni msingi muhimu katika kuunda mazingira bora kwa ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini. Katika awamu ya pili, **malengo** yaliyopangwa ni:

- Kuhakikisha kuna utaratibu na mfumo unaozingatia utawala wa sheria, demokrasia, uadilifu, ufanisi, uwajibikaji, uwazi, shirikishi na kupunguza rushwa.
- Kuongeza utoaji wa huduma za jamii kwa wote, hasa kwa watu masikini na makundi ya watu wenye mahitaji maalum.
- Kuongeza ulinzi wa haki za binadamu kwa wote na hasa wanawake, watoto na wanaume masikini. Wengine ni makundi yenye mahitaji maalum wakiwemo wazee na watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU).
- Kuimarisha ulinzi wa watu na mali zao na usalama wa taifa.
- Kukuza na kuendeleza utamaduni wa uzalendo, kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujiamini.

9.0 MPANGO WA UTEKELEZAJI

9.1 Mchakato wa Kuratibu Mabadiliko ya Programu

Serikali imeandaa mchakato wa kuratibu mabadiliko ya utekelezaji. Lengo ni kukuza ufanisi wa utoaji huduma kwenye ngazi mbalimbali. Mfano, mchakato wa Ukaguzi wa Matumizi ya Fedha za Umma utaendelea kujadiliwa na kupewa kipaumbele.

Ili kuboresha zaidi shughuli za uratibu, serikali imeshaanza kutumia mwongozo wa Mpango Mkakati wa Kati. Mwongozo huu ni muhimu katika kufanya tathmini, kupanga mipango, bajeti na kuandaa ripoti. Mwongozo huo utaendelea kutumiwa na Wizara, Idara na wakala wa Serikali (MDAs).

Katika kuhakikisha kwamba mwongozo huo utatumika ipasavyo, Wizara ya Fedha itachukua hatua zifuatazo;

- ✓ Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wanaoshughulikia mipango, bajeti, usimamizi na kuandaa ripoti.
- ✓ Kuzingatia viwango na misingi iliyomo ndani ya mwongozo huo.
- ✓ Kutoa taarifa na kuimarisha kamati za bajeti.
- ✓ Kuzipa jukumu wakala na idara za Sera na Mipango kuhakiki utekelezaji wa yaliyoagizwa ndani ya mwongozo na kuripoti Wizara ya Fedha.

9.2 Ushirikishwaji wa Taasisi za Serikali

Ili kufanikisha utekelezaji wa MKUKUTA II na kupata matokeo tarajiwa, jitihada zaidi zinahitajika katika kuratibu shughuli za wadau wote. Hatua zifuatazo ni muhimu katika kuhakikisha ushiriki;

- ✓ Kuimarisha uwezo wa taasisi za serikali; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Mipango, Baraza la Mawaziri, Tawala za Mikoa na Kamati za Maendeleo za Wilaya zenye wajibu wa kuratibu sera.
- ✓ Kuimarisha utoaji na upatikanaji wa taarifa katika ngazi zote za serikali.
- ✓ Kutenga fedha kwa ajili ya uratibu na mifumo shirikishi.
- ✓ Uchambuzi wa namna ya ushiriki na kuunganisha masuala ya kisekta yanayoendana.
- ✓ Kutoa taarifa kuhusu sehemu na maeneo ambapo programu/miradi inatekelezwa.

9.3 Ushirikishaji Umma na Taasisi Binafsi

Serikali imechukua hatua mbalimbali kuongeza ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa MKUKUTA II na masuala ya fedha. Utekelezaji wa vipaumbele vya kukuza uchumi unahitaji fedha na rasilimali nyingi. Serikali pekee haiwezi kukidhi mahitaji.

Wananchi ni moja ya wadau wa maendeleo. Hawana budi kushirikishwa kwenye utekelezwaji wa kukuza uchumi.

Kwa kutambua changamoto hiyo, serikali itaiomba sekta binafsi kushiriki kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kipaumbele.

Baadhi ya maeneo hayo ni afya, elimu, kilimo, maji, mazingira, nishati, makazi bora, usafirishaji na miundombinu. Mengine ni chakula na lishe, ajira endelevu, utalii, utamaduni na michezo. Mengine yanayohitaji rasilimali zaidi ni ustawi wa jamii, utawala bora na uwajibikaji, ardhi, usalama wa watu na mali zao na ulinzi wa haki za watu wa makundi maalum.

Serikali pia itapanua fursa ya mijadala kati yake, umma na taasisi binafsi. Vilevile itaweka vivutio na mifumo ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na kuhakikisha kuwa watu masikini wananufaika na uzalishaji.

9.4 Kujenga Uwezo

Serikali na wadau wanatambua kwamba kujenga uwezo wa watendaji katika ngazi mbalimbali ni suala linalohitaji kupewa kipaumbele. Maeneo yaliyotambuliwa ni katika uongozi, uchambuzi na uundaji sera, mpango mkakati, utekelezaji, uratibu, usimamizi na kufanya tathmini. Maeneo mengine ya kipaumbele ni;

- ✓ Kuongeza zaidi fedha, vifaa na rasilimali watu kwa mamlaka za serikali za mitaa.
- ✓ Kujenga uwezo zaidi kwenye maeneo ya ununuzi, mikataba na usimamizi wa program na miradi.
- ✓ Kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo kazini, kubadilishana uzoefu kwa kujifunza kutoka Ushirikiano wa nchi za Kusini, mafunzo ya muda mrefu nk.
- ✓ Kuboresha mazingira kwa ajili ya ukuaji wa sekta binafsi na kuongeza nafasi ya mashirika ya hiyari kama wadau wa serikali katika kutoa huduma.
- ✓ Kuendelea kuwasaidia wajasiriamali wadogo hususan katika kuwapatia mikopo, masoko na maeneo ya kufanyia biashara.

9.5 Msaada wa Kiufundi

Mpango mkakati wa kitaifa wa Msaada wa Kiufundi una lenga katika kujenga uwezo; jinsi ya kupata msaada wa kiufundi, kusimamia na kutathmini mipango na program mbalimbali za

maendeleo. Mpango huu utaanza kwa kuandaa na kutekeleza sera ya taifa ya Msaada wa Kiufundi, kuandaa mkakati na mpango kazi wake pamoja na kuhakikisha kuwa unafanya kazi kwa manufaa ya nchi.

9.6 Kukuza Ajira

Suala la kuwa na ajira endelevu linatiliwa mkazo katika utekelezaji wa MKUKUTA II hasa ikizingatiwa kuwa ajira ni kiungo muhimu kwenye ukuaji wa uchumi.

10.0 USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MKUKUTA II

Kwa ujumla, dhumuni la kufuatilia utekelezaji wa MKUKUTA II ni kuona kwamba fursa ya majadiliano ya kisera kuhusu ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini inakuwepo. Ufuatiliaji wa MKUKUTA II utahakikisha;

- Takwimu sahihi kwa ajili ya ufuatiliaji wa ukuaji uchumi na kupunguza umaskini zinapatikana kwa wakati.
- Kuna juhudi za ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu na kuhimiza matumizi yake miongoni mwa wadau wa maendeleo.
- Kukuza na kuandaa mipango, bajeti na maamuzi thabiti katika ngazi zote za serikali.
- Matokeo ya tafiti na uchambuzi wa takwimu zinasambazwa kwa wadau wengi zaidi.
- Uchambuzi wa kina wa takwimu za ukuaji na mwenendo wa umaskini unafanyika.
- Malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa yaliyoridhiwa na Tanzania yanajumuishwa na kufuatiliwa kama sehemu ya utekelezaji wa MKUKUTA II.

11.0 USIMAMIZI WA FEDHA

MKUKUTA II haiwezi kufikia malengo yaliyopangwa bila kuwa na fedha. Hivyo basi, serikali imeainisha mfumo maalum wa upatikanaji na matumizi ya fedha yatakayochochea ukuaji uchumi mkubwa na mdogo. Inakadiriwa kwamba pato la taifa litaongezeka kutoka asilimia 15.7 mwaka 2009/10 hadi kufikia asilimia 21.8 mwaka 2014/15.

Matarajio ya ukuaji ni kwamba;

- Uchumi wa ndani utandelea kuimarika baada ya mtikisiko mkubwa wa uchumi wa dunia
- Makusanyo ya kodi ya ndani yataimarishwa
- Mpango wa Kilimo Kwanza utaendelezwa
- Mazingira ya biashara yataboreshwa zaidi
- Ubia kati ya sekta binafsi, wananchi na serikali utaimarishwa
- Usimamizi na tathmini ya matumizi ya rasilimali za umma utaboreshwa
- Utulivu na uvumilivu wa kisiasa utandelezwa
- Kunakuwepo sera ya uchumi itakayopunguza mfumuko wa bei, kushusha riba na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi

Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa MKUKUTA II zitatokana na;

- Mapato ya ndani; makusanyo ya kodi mbalimbali.
- Fedha na mikopo zitakazotokana na ubia kati ya serikali na sekta binafsi.
- Misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo kupitia miradi au programu zinazochangia ukuaji uchumi.

Hata hivyo, utekelezaji wa MKUKUTA II unaweza kuathirika iwapo:

- Uchumi wa dunia utakua kwa kasi ndogo.
- Bei za mafuta ya dizeli na petroli itaendelea kupanda.
- Uharamia unaoendelea kwenye bahari ya Hindi hautakomeshwa. Hali hiyo itaathiri vibaya biashara na mauzo ya ndani na nje.
- Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (EURO) itaendelea kutetereka na kusababisha kupungua kwa misaada.

12.0 MAJUKUMU NA WAJIBU WA MWANANCHI NA TAASISI MBALIMBALI

Ili kufanikisha MKUKUTA II, ni jukumu na wajibu wa kila mwanajamii kushiriki. Wafanyabiashara, wakulima, wavuvi, wazalishaji, mashirika ya hiyari, viongozi wa ngazi zote na wadau wa maendeleo wana jukumu la kushiriki kwa vitendo, kusimamia utekelezaji na kutathmini maendeleo ya MKUKUTA. *Mwananchi,* shiriki kwa kufanya yafuatayo:

- Soma na kuyaelewa vyema malengo ya MKUKUTA.
- Fuatilia kuanzia ngazi ya kitongoji/mtaa, kata, tarafa,

wilaya hadi ngazi ya mkoa kuhakikisha huduma bora za jamii zinatolewa.
- Jihusishe katika shughuli za maendeleo; serikali za mitaa, kamati za shule, vyama vya ushirika, vikundi vya biashara, uvuvi, kilimo nk.
- Tafuta habari za maendeleo ya malengo ya MKUKUTA kutoka kwenye vyanzo mbalimbali; taasisi za umma, vyombo vya habari, wabunge, madiwani, asasi za kiraia, asasi za kidini, vyama vya wafanyakazi na ushirika, wadau wa maendeleo na sekta binafsi.
- Hakikisha viongozi kuanzia ngazi ya jamii, wilayani hadi taifa wanawajibika.

Wizara mbalimbali nazo pia zina wajibu na majukumu katika utekelezaji wa MKUKUTA II:
- Kutoa mtazamo na mwelekeo wa utakelezaji wa MKUKUTA II.
- Wizara inayoshughulikia masuala ya uchumi itasimamia na kuhakikisha kuna mazingira mazuri yatakayowezesha utekelezaji wa MKUKUTA II.
- Wizara ya Fedha itafuatilia na kukusanya fedha kwa ajili ya utekelezaji.
- Wizara ya Utumishi wa Umma itaratibu programu za kujenga uwezo na kuongeza ujuzi.
- Wizara inayoshughulikia serikali za mitaa itaratibu utekelezaji wa programu katika ngazi za mikoa na wilaya. Wizara hiyo pia itasimamia mafunzo ya kujenga uwezo, kukusanya na kusambaza taarifa kutoka ngazi ya chini hadi taifa na kutoka ngazi ya taifa kuzirudisha chini.

Taasisi binafsi:
- Zitafanya kazi kwa karibu na serikali kuzalisha bidhaa na kuendeleza masoko ambayo yatawanufaisha watu masikini.
- Kukuza maendeleo ya sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali.
- Kusaidia kutafuta fedha kwa ajili ya kazi za MKUKUTA II ambazo ziko chini ya sekta binafsi kama vile mikopo.
- Kuongeza kazi na ajira endelevu
- Kupanua ushiriki wa umma na taasisi binafsi katika midahalo ya uundaji wa sera kwa kushirikiana na serikali.
- Kushiriki katika vita ya kupambana na rushwa na kujenga mazingira sawa ya kibiashara.

- Kutafuta na kuibua fursa za maeneo ya uwekezaji ndani ya nchi, Afrika Mashariki na nchi nyingine.
- Kuhamasisha sekta binafsi kulipa kodi zinazostahili.

Mashirika ya hiyari: Ni wadau muhimu katika harakati za kupunguza umasikini. Wajibu na majukumu yao yatakuwa:

- Kujenga uwezo na kuiwezesha jamii kushiriki katika kusimamia na kutathmini utekelezaji katika ngazi ya jamii hadi taifa.
- Kuchochea uwajibikaji wa viongozi wa mashirika ya hiyari na wa serikali kwa wananchi.
- Kufanya kazi kwa karibu na wizara na serikali za mitaa ili kuhakikisha kuwa masuala mtambuka (yanayogusa sekta zote) yamezingatiwa katika mipango ya utekelezaji ya kisekta na ile ya wilaya.
- Kutathmini na kuimarisha uwezo wa mashirika ya hiyari kuanzia ngazi ya jamii, wilaya hadi taifa.

REJEA:

1. **Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA 2009/10** *(Mdahalo kuhusu sera za Kitaifa-Tarehe 2-8 Desemba, Blue Pearl Hoteli-Ubungo Plaza, Dar es Salaam).*
2. **National Strategy for Growth and Reduction of Poverty II** (NSGRP II), Ministry of Finance and Economic Affairs, July 2010.

VIFUPISHO

MKUKUTA	Mkakati wa kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MEMKWA	Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala za Serikali
NGOs	Mashirika ya Kiraia (Non- Govermental Organisations)
TEKNOHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
VVU	Virusi Vya Ukimwi

Je, una maoni au ushauri? Wasiliana nasi kupitia:

policy forum

Kitalu 270 KIKO AVENUE Mikocheni B
S.L.P 38486 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2772611/+255 782 317434
Nukushi: + 255 22 2701433